



Mkoa wa Singida.
Simu Na. 0262502252/2237
Fax Na. 0262502719
Barua pepe: ded.singidadc@singida.go.tz

S.L.P. 27,
SINGIDA.

Kumb. Na. SDC/B.1/50/PART"E"/136

Tarehe: 26/09/2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Singida imepata idhini ya utekelezaji wa Ajira Mpya katika mwaka wa fedha 2021/2022 kwa barua yenye Kumb. Na.FA.170/366/01"B"/59 ya Tarehe 02/09/2022 kutoka kwa Katibu Mkuu- UTUMISHI.

Hivyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Singida anawatangazia watazania wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya Singida, kuomba nafasi za kazi zifuatazo kwa masharti ya kudumu kuanzia leo tarehe 26/09/2022:

2.0 MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II (Nafasi 02)

2.1 SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe na elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI)
- Awe na Astashahada/cheti NTA Level 5 cha mafunzo ya utunzaji kumbukumbu katika mojawapo ya fani za Afya au Masijala.

2.2 KAZI/ MAJUKUMU YA MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU

- i. Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/majalada yanayohitajiwa na wasomaji
- ii. Kudhibiti upokeaji, uandikishaji wa kumbukumbu/nyaraka za Ofisi.
- iii. Kuchambua, kuorodhesha na kupanga kumbukumbu/nyaraka katika makundi kulingana na somo husika (**Classification and Boxing**) kwa ajili ya matumizi ya Ofisi.
- iv. Kuweka, kupanga kumbukumbu/nyaraka katika reki (file racks/cabinet) katika masjala/vyumba vya kuhifadhia kumbukumbu.
- v. Kuweka kumbukumbu (barua,nyaraka n.k) katika majalada.
- vi. Kushughulikia maombi ya kumbukumbu/nyaraka kutoka Taasisi za Serikali na
- vii. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi.

2.3 MSHAHARA

- Kwa kuzingatia Ngazi ya Mishahara ya Serikali, yaani TGS B.


2.4 MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

- i. Muombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- ii. Muombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa.
- iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) wawili.
- iv. Maombi yote yaambatane na picha 2 (passport size), nakala za vyeti vya taaluma vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa zilizoelekezwa hapo juu.
- v. Waombaji wote waambatanishe nakala ya kitambulisho cha Taifa (NIDA) kwa ambao hawana vitambulisho hivyo, namba za nida ziandikwe kwenye maelezo binafsi (CV).
- vi. "Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.
- vii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU au NECTA).
- viii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali cha Mamlaka husika.
- ix. Barua ya maombi iandikwe kwa lugha ya Kiswahili au Kingereza
- x. Waombaji watakaokidhi sifa ndio watakao itwa katika usaili
- xi. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.
- xii. Maombi yote yatumwe kwenye anuani ifuatayo;

Mkurugenzi wa Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P 27,
SINGIDA.

**N:B Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 09 Oktoba, 2022 saa 9.30
alasisiri.**

Imetolewa na:


Ester Chaula
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
SINGIDA

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
SINGIDA**

Nakala: Katibu,
Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
S.L.P. 2320,
DODOMA.

Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira www.ajira.go.tz

Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya Singida
Singidadc.go.tz

Mbao za Matangazo